



## KWA AJILI YA VIJANA

# Epuka Marafiki Wabaya!

**Maagizo:** Fanya zoezi hili katika mazingira matulivu. Unaposoma maandiko, jiwazie ukiwa katika matukio yanayozungumziwa. Wazia kikao. Sikia sauti. Hisi kama wahusika wakuu wanavyohisi. Wazia kwamba masimulizi haya ni halisi kabisa.

**Wahusika wakuu:** Dina, Shekemu, Yakobo, Simeoni, na Lawi

**Muhtasari:** Dina ananajisiwa na Shekemu, na ndugu zake wenye hasira wanalipiza kisasi.

### ❶ CHUNGUZA TUKIO HILI.—SOMA MWANZO 34:1-31.

Unafikiri Dina alijihusisha na mambo gani akiwa na rafiki zake huko Kanaani?

---

---

---

Unafikiri ni maneno gani yenye ‘kushawishi’ ambayo Shekemu aliendelea ku-mwambia Dina?

---

---

Unatambua hisia gani wakati Yakobo anapowakemea Simeoni na Lawi katika mstari wa 30?

---

---

### ❷ CHIMBA ZAIDI.

Unafikiri ni kwa nini Dina aliwatembelea mabinti wa Kanaani kwa ukawaida? (Kwa mfano, walishirikiana katika mambo gani? Alipata vitu gani miongoni mwa Wakanaani ambavyo hangeweza kupata kwao nyumbani?)

---

---

Ni sifa gani zenye kuvutia za Shekemu ambazo huenda Dina aliona? (*Soma tena mstari wa 3, 12, na 19.*)

---

---

Biblia inaonyeshaje kwamba Dina hakutaka kufanya ngono na Shekemu? (Soma tena mstari wa 2.)

---

---

Unafikiri ilikuwa sawa kwa Simeoni na Lawi kulipiza kisasi kwa kuwauwa wanaume wa jiji la Shekemu? Kwa nini?

---

---

**3 TUMIA MAMBO ULIYOJIFUNZA. ANDIKA MAMBO ULIYOJIFUNZA KUHUSU . . .**

Umuhimu wa kuchagua rafiki zako kwa busara.

---

---

Umuhimu wa kujizuia, hata kama una sababu nzuri ya kukasirika.

---

---

**NJIA NYINGINE UNAYOWEZA KUTUMIA HABARI HIYO.**

Unaweza kufanya nini ili kuepuka kutumiwa vibaya kingono na watu ambao hawathamini viwango vya Mungu vya maadili?

---

---

**4 NI MAMBO GANI KATIKA SIMULIZI HILI AMBAYO YAMEKUGUSA MOYO SANA, NA KWA NINI?**

---

---

---

